

HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA

(BaruazotezitimwekwaMkurugenziMtendajiWilaya)

Tel. 028280 4865

Fax. 028280 2719/2370

Email: Ded@Kigomadc.Go.Tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,

S.L.P. 332,

Kigoma.

Kumb. Na. KDC / C1 / 36/98

Tarehe: 06 Machi 2023

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma anapenda kuwatangazia Watanzania wote kuwa ofisi imepoke kibali cha Ajira Mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu **UTUMISHI** chenye **Kumb.Na.FA.170/358/01"C"/136** cha tarehe 13.01. 2023 kwa ajili ya kutangaza nafasi ya kazi ya **Msaidizi wa Kumbukumbu II** kwa masharti ya kudumu. Hivyo Watanzania wote wenye sifa mnaombwa kuomba nafasi hiyo kama ifuatavyo:

1. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU II - NAFASI MOJA (1).

i. SIFA ZA KITAALUMA KWA MWOMBAJI

Kuajiliwa wenye Stashahada (NTA level 6) katika fani ya Masijala, Urasimu Ramani (cartography) au (geoinformatics), Sheria, au Afya kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Selikari wenye Ujuzi wa Kompyuta.

ii. MAJUKUMU YA KUFANYA:

- Kuthibiti mifumo ya kumbukumbu, kutunza, na kusimamia matumizi ya kumbukumbu za Halmashauri ya Wilaya.
- Kutambua na kutafuta kumbukumbu katika masijala ya Halmashauri ya Wilaya.
- Kuthibiti mfumo wa kumbukumbu zinazozalishwa na kompyuta, kutunza na kusimamia matumizi yake katika Halmashauri ya Wilaya.
- Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya Taasisi (File Tracking).
- Kupokea majalada yanayorudi Msijala toka kwa watendaji.

iii. MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- Mwombaji awe ni raia wa Tanzania na mwenye Akili Timamu
- Awe na umri wa miaka 18 na asiyezidi miaka 45.
- Maombi yote yaambatane na vivuli (photocopies) vya vyeti vya Taaluma, ujuzi, Cheti cha kuzaliwa, picha mbili (02) passport size) za rangi za hivi karibuni.
- Waombaji wote waambatanishe wasifu wasifu wenye maelezo binafsi yanayojitoshesheza (Detailed CV) yenyen anuani na namba za simu za kuaminika.
- Waombaji waliosoma nje ya nchi wahakikishe vyeti vyao vinahakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).
- Maombi yaandikwe kwa Lugha ya Kiswahili au Kiingereza.

- g) Waombaji wa kazi ambao tayari ni waajiliwa katika utumishi wa umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelezo yaliyopo katika waraka Na. CAC45/257/01/D/140 wa Tarehe 30/11/2020.
- h) Waombaji waliostaafu utumishi wa umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama anakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- i) Awe hajawahi kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai.
- j) Awe na kitambulisho cha Uraia (NIDA) au namba ya kitambulisho hicho.

iv. MASHARTI YA AJIRA:

Ajira ya kudumu.

v. NGAZI YA MSHAHARA:

Ngazi ya Mshahara wa kuanzia ni TGS C1.

MAOMBI YOTE YATUMWE KWA ANUANI ZIFUATAZO

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri Ya Wlaya Ya Kigoma,
S.L.P 332,
Kigoma.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 21/03/2023 saa tisa na nusu (09:30p.m) Alasiri.

Tangazo linapatikana katika tovuti ya Halmashauri ambayo ni www.kigomadc.go.tz, tovuti ya secretarieti ya ajira www.ajira.go.tz na katika mbao za matangazo za halmashauri ya Kigoma.

Tangazo hili limetolewa na



Rose R. Manumba

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KIGOMA**